**MWONGOZO WA FASIHI SIMULIZI**

**SEHEMU YA A:USHAIRI**

a) Kichwa

Kielelezo kibaya
Tabia mbovu kwa watoto
Wazazi wabaya/ walegevu

b) Maudhui ya shairi

Mshairi anasema kuwa wazazi wanahasiri watoto kwa pupa yao ya kulewa kila wakati na kuwa kielelzo kibaya
Wazazi kukaa vilabuni mpaka usiku wa manane bila kufahamiana na watoto wao ni vibaya
Wazazi kuwapa watoto pesa nyingi ni tabia potovu kwani wanazitumia dawa za kulevya
Wazazi wanatafuta utajiri na kukosa wakati wa kuwashauri/ kuwafunza maadili mema

c) Kinachojenga ukuta

Hapana mazungumzo ya kishauri baina ya watoto na wazazi nah ii hujenga ukuta baina ya watoto na wazazi
Kulewa kila wakati na kukaa kilabuni kwa mpaka usiku wa manane hujenga ukuta kwa kuwa mzazi huwa hapati wakati wa kuzungumza na mtoto 2x1=2

d) Tamatahli za usemi

i. Takriri – ni sumu, sumu
ii. Tashihisi – ndoto zinajenga ukuta/ yanakufunga katika klabu
iii. Istiara – ni sumu Kutaja – 1, Mfano – 1

e) Umbo la shairi

Lina beti nne
Kila mshororo una mishororo tisa isipokuwa ubeti wa mwisho
Ni shairi huru kwa kuwa halizingatii arudhi

f) Lugha nathari- ubeti wa nne

i. Mshairi anasema kuwa wazazi wanaumiza watoto kwa kuwapa pesa
ii. Ni vibaya kuliwaza watoto kwa kuwapa pesa
iii. Kwani huwaingiza katika maovu ya kuvuta sigara na ulevi na mihadarati
iv. Hali hii inaishia upotofu wa watoto/ huwaingiza katika hali mbaya/ kifo

g) Maana ya vifungu

i. Giza baridi – hali mbaya/ kifo
ii. Yanakufunga katika klabu – kuwa na mazoea mabaya ya kukaa kilabuni kulewa mpaka usiku wa manane

**SEHEMU YA B:RIWAYA KIDAGAA KIMEMWOZEA**

**2.** sokomoko ni hali ya heka heka na ghasia.kusokomeza ni kulazimisha mambo.jina hili linaafiki kwani: i) kunatokea mauaji ya yusufu, wakoloni n.k
ii) unyakuzi wa mali ya umma
iii)viongozi kuendeleza ufisadi
iv)upujufu wa kimaadili.(mapenzi na motto mdogo)
v)ukiukaji wa haki za kibinadamu(motto kutupwa na kuwashinikisha wengine kumlea)
vi) wizi wa mawazo(majisifu)
vii) wasomi wanashindwa kuyadhibiti maisha yao(majisifu)
viii)kusambaratika kwa familia
ix)dhiki za watu wenye mahitaji maalum(Dora kuwafungia watoto wageni wanapotembea)
x)usaliti wa kimapenzi(michelle)
xi)mahakama kutumiwa kamachombo cha ukandamizaji.(yusufu kufungwa bila hatia)
xi)ubaguzi wa kikataba
kuuawa kwa paka kikatili.n.k

**3**. a) ni nyumbani mwa nasaba Bora, chumbani mwa malazi.Nasaba Bora ndiye aliyesimama

anawatazama Bi Zuhura naamani ambao wamefumaniwa chumbani alipomwita Amani.anaamua kuwa wanamwendea kinyume na kumpiga Amani kikatili.

b) Tashbihi :kutetemeka kama waliopigwa na dhoruba ya theluji
   Taswira : kauli inasawiri picha ya wahusika wanaotetemeka kwa woga.
   Chuku : woga wa bi Zuhura na amani unatiliwa chumvi ili kusisitiza hatari inayowakabili.

c) umuhimu wa nasaba bora
   i) anawakilisha ufisadi wa viongozi
   ii) ni kielelezo cha waafrika wanaorithi na kuendeleza sera hasi za uongozi.
   iii) anafanyia tastiti mapuuzo ya viongozi.anapuuza kunadhifisha kasri lake na kuwafuta kazi wafanyakazi wanaojaribu kulinadhifisha.
   iv) anaendeleza ukiukaji wa haki za watoo kwa kumtupa motto.
   v) kupitia kwake mshikamano ya kijamii unasisitizwa hasa katika mazishi mkewe anahudhulia.
   vi) upujufu wake wa kimaadili ndio unaosababisha kusambaratika kwa ndoa yake.
   vii) ndiye kichocheo kikuu cha kuvunjika kwa uchumba kati ya Mashaka na Ben Bella.
   viii) kupitia kwake sifa za wahusika zinachimuzwa,kama utu wa Amani na usamehevu wa Bi Zuhura.
   ix) udhalimu wake ndio unaomhamasisha Madhubuti kubadilika na kuungana na Amani kujenga jamii mpya.

**SEHEMU YA C:TAMTHILIA MSTAHIKI MEYA**

**4. a)** maneno yalisemwa na Meya kwa diwani III wakiwaofisini kwa meya.diwani III alikua amefika kwa mwaliko wa Meya.Meya amemwita kumwelezea kuwa madiwani wanahitaji kuongezwa mishahara.

b) nyakati zingine walizotofautiana.

- Wakati ambao wafanyakazi wa cheneo waligoma meya alisema kuwa wangerudi kazi kwani mhitaji ni mtumwa.Diwani III alisema wangewahitaji wale wafanyikazi na waliwalipa kwa walioifanya na alifafikiria si watumwa.
- Kuajiri vijana wengine ktk nafasi ya wanaogoma aliona si vyema na tena itachukua muda kuwafunza
- Kuongezewa marupurupu kwa walinda usalama anasema baraza la cheneo haliwezi kuwatosheleza.
- Kuto lipa kodi kwa madiwani ni kuongeza nakisi iliyoko ya milioni moja ishirini na meya kumweleza atafute namna ya kufidia nakisi hiyo.
- Kuhusu uzalendo madiwani wengine wanakubaliana watu waimbiwe nyimbo za kizalendo naanasema nyimbo hazitafaa na kitakachofaa ni kuwasikiliza.
- Uongo kuhusu dawa anapendekeza wasipewe ahadi za bure.
- Mikopo kutoka ngambo anasema ni suluhisho kwa matatizo yao lakini ni mzigo mkumbwa wange waachia wajukuu wao.
- Kubuniwa kwa kamati alisema kamati hizo huenda siziwe na umuhimu.

**5.** njia za meya za kuuendeleza uongozi wake

- Idhaa ya baraza: ili kuamsha uzalendo, tamasha ya vijana kuandaliwa na kutuzwa.mashindano hayo kuonyeswa moja kwa moja.
- Sheria: Mayors' Act ilimpa Meya mamlaka kumchukulia mtu yeyote hatua.pia Riots Act ilimpa meya nguvu.
- Vibaraka: kama bili, Diwani wa I na II walitumiwa kuendeleza uongozi dhalimu.
- Ahadi za uongo:
- Askari: wanatumiwa kutawanya wafanyi kazi.
- Dini: mhubili kuliombea baraza na kumuunga mkono.
- Uundaji wa kamati.
- Hongo: anasema madiwanin wana njaa na wasitozwe kodi wengine wakitoshwa.muhubiri kupewa pesa za sadaka laki moja kila mwezi.
- Vitisho;
- Tenga utawale; Meya anamtenga diwani wa III kwa sababu ya kuwatetea wanyinge nakuipinga mipango ya Meeya.

- Propaganda: redio kucheza nyimbo za uzalendo ili kuwazinikisha watu kuamini kuwa kila kitu ki sawa.

(Mtahiniwa aeleze zote 10)

**SEHEMU YA D:HADITHI FUPI DAMU NYEUSI**

**6.a)**msemaji ni Aziza akimjibu mumewe.msimulizi alikuwa ameamua kumtoa Aziza kutoka tabia zake za ushamba.alimuuliza sababu za kutovaa viatu na alikua na vya kila aina na akasema kuwa mguu wake ni mgumu na hauwezi ukandukika mwiba.

b) sifa za aziza;

- **Mwelevu**
- Mwenye bezo;aliudunisha mswaki alionunuliwa akisema ni manyoya ya nguruwe.
- Jasiri: aliamua kumweleza mumewe yote aliyofikilia kumhusu na hata kumwita mume gumegume bila woga.
- Anayechuja mambo:daima alimwangalia mumewe kama kwamba anamchuja.
- Ana msimamo dhabiti: alishikilia mawazo yake kuhusu mume bora na kumwita muuza madafu ili athibitishe kuwa lazima mume amlishe na amtunze mke.
- Mkomavu: amekomaa.hawezi kuendeshwa kama alivyofikilia msimulizi.

**Umuhimu**

**i)** Kielelezo cha wana wake jasiri na ambao hawakubali kudhalilishwa.

ii) kielelezo cha wanawake hawajapata elimu lakini bado ni werevu/watambuzi hasa kuhusu mambo ya maisha

**7.a) ubaguzi**

1. **Damu nyeusi**

   Watu weusi kubaguliwa katika nchi ya weupe.fikirini aliachwa ktk kituo cha basi kwa sababu ni mweusi

   Waafrika weusi walibaguliwa na wamarekani waliowatapeli.

   Wahadhiri vyuoni walionyesha ubaguzi

   Walinzi madukani walionyesha ubaguzi,walimshuku Fikirini kuwa angedokoa vitu kwa sababu alikuwa ni mweusi.

   Weusi walitozwa faini kwa kuvuka barabara taa zikiwa nyekundu na wazungu hawapewi adhabu.

2. **Maskini Babu Yangu**

   Watantele wanawabagua wasio na rangi kama yao.ndio sababu wanawake watantele walimshuku Babu Maende na hatimaye alipigwa kitutu.

   Wamidi hawatangamani sana na makabila mengine.

   Maskini wamebaguliwa na wanaishi ktk mitaa madongoporomoka.wanaoishi ktk kijiji cha kochokocho hali yao ilikuwa ni ya ukuta.

   Wanakijiji hawana huduma sawa na walio mjini.

**b)ndoa**

**1.Maeko**

- Mateso ambayo Jamila ahayakumfanya aasi ndoa hii
- Ndoa ya hamduni na jamila inaonekana Hamduni akiwa na sifa mbili moja akilewa ni mkatili na akilevuka alikuwa mume mwenye mapenzi
- Jamila aliadhilika kutokana na vipigo alivyopata ktk mwili wake.kisaikolojia aliathilika kwani alikuwa na upweke kutokana na kusemwa na watu.
- Ndoa ina mapenzi kwani Jamila alimpenda Duni sana
- Katika ndoa kunayale maeko ambayo watu hawawezi kuyaelewa.

**2.Mke wangu**

- Msimulizi alikuwa na vigezo vyake vya kuchagua mchumba
- Wazazi walikuwa najukumu ya kuchagulia watoto wao wachumba.
- Aziza hakuwa na nafasi ya kutimiza wajibu wake kama mke kwa kuwa waliishi ktk kivuli cha wazazi wa Msimulizi.
- Wachumba wote wawili hawakusikizana na Aziza hakuwa na furaha.
- Msimulizi alisema kuwa kuowa mke amesoma kulileta maafa ktk ndoa za wenzake.

**3.Ndoa ya samani**

- Haikuwa na mapenzi bali tamaa kwa upande wa Amali na familia yake.
- Ndoa haikukamilika kwani Abu aligundua kuwa Amli na familia yake walitaka pesa

**c)umaskini**

**1. kanda la usufi.**

- Makao duni.nyumba waliolala Kadogo na Rozina ilikuwa ya msonge na ilitumiwa kama jikoni.
- Mamake Sela hangeweza kumnunulia Kadogo nguo na alimvisha matabara.

- Mzee Butali alitumia pesa zake kumwelimisha Sela mpaka akaitwa pangu pakavu.
- Chris hakuweza kumudu pesa za kutimiza taratibu za mila za kulipa mahari
- Kazi ya kukata mikonge aliyoifanya Chris ilikuwa na mshahara duni

**2.Maskini Babu Yangu**

- Watu waliishi ktk mabanda ambayo yalikuwa karibu kuporomoka
- Mazingira machafu sana
- Mtaa wa Kochokocho uliishi watu duni kutoka makabila tofauti tofauti na walikuwa wachochole.
- Watu walipikia nje na kuuza vyakula vile ktk mazingira machafu.

**SEHEMU YA E:FASIHI SIMULIZI.**

**8**.a) Sifa za mtambaji bora

- Awe na uwezo wa kuwasilisha hadithi.
- Anafaa kutumia njia inayochangamsha hadhira.
- Awe na ujuzi wa kuifahamu hadhira yake.
- Awe na ufahamu mpana wa lugha pamoja na utamaduni unaohusika.
- Awe na uwezo wa ufaraguzi.
- Aweze kufahamu tabia za binadamu na mikondo mbalimbali ya jamii. 5 x 2 = 10

b) Wajibu wa nyimbo

- Hutumbuiza
- Kuwasifu watu maarufu
- Kusahihisha maovu ya jamii
- Huhifahi utamaduni
- Huelimisha watu
- Hukuza lugha
- Huhamasisha watu
- Kufariji waliofiwa
- Kuendeleza uhai wa jamii n.k (1 x 4)

c) i) Kitendawili ni fumbo/msemo wa kinafumbo amabao hufumbua jambo Fulani na hutolewa hadhira au wasikilizaji ili waufumbue. 1 x 2= 2

ii) Hutangulizwa kwa njia maalumu

a) Ujumbe wake ni wa kimafumbo

b) Ufananisho wa kihazanda

c) Ni fupi kwa maelezo

d) Hutegemea mazingira/sehemu Fulani 4 x 1 = 4

**9**.a) i) Visasili - Hadithi zinazosimulia asili ya watu, vitu ama tabia Fulani.

ii) Ngano za mazimwi - Husimulia kuhusu mazimwi

iii) Hurafa - Hadithi ambazo zina wahusika wanyama lakini waliopewa tabia za binadamu.

iv) Hekaya - Ngano fupi zinazosimulia matukio ya kushangaza yanayoonyesha hila au ujanja wa mwanadamu

v) Mighani - Ngano za ushujaa
Mighani huwa na lengo la kueleza visa na mikasa ya watu ama mashujaa wa jamii fulani.

b) i) Kutumia viungo vyake vya mwili kuikuza na kuifanya hadithi kusisimua.

ii) Msimuliaji kuchukua nafasi ya wahusika katika hadithi ili kuishirikisha hadhira.

iii) Uwezo wa kuiga matendo na wahusika kwa kuimba na kupiga makofi ili kuvutia hadhira.

iv) Ucheshi na mvuto wa lugha ili kuifanya hadhira kushikika.

c) i) Majigambo – Mazungumzo yanayotolewa na mtu fulani ili kutapa

ii) Mivigha – sherehe maalum za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii katika kipindi maalum.

iii) Lakabu – Majina ya utani au kupanga ambayo watu hujipa au kupewa